TANGAZO LA SERIKALI NA. 412 la tarehe 24/05/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2024

Jina

1.- Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2024.

Matumizi

2.- Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Same.

Tafsiri

3.- Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauriya Wilaya ya Same;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa

Halmashauri ya wilaya ya Same au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mchimba madini" maana yake ni mtu mwenye kibali kutoka mamlaka husika, kinachomhalalisha kumiliki eneo lililotengwa kwa ajili ya kuchimba madini ya ujenzi;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

Sura ya 290

"Sheria" maana yake ni sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazotolewa katika eneo la halmashauri; na

"wakala" maana yake mtu binafsi, kikundi, taasisi, kampuni au asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru au ada kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Maombi ya kibali

4.-(1) Taasisi, kampuni au mtu yeyote

anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kwa kujaza fomu maalum itakayotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika;

(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;

(c) umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;

(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na

(e) muhtasari wa kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukionesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(3) Mkurugenzi, ndani ya muda wa siku saba tangu kupokea maombi, atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za uchimbaji.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (3) Mkurugenzi baada ya kukamilika

kwa ukaguzi wa eneo linaloombewa kibali atatakiwa kukubali au kukataa maombi na iwapo atakataa atatoa sababu za kukataa maombi hayo.

Wajibu wa mwenye lesenikibali

5.- Taasisi, kampuni au mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atatakiwa:

(a) kuomba kibali kama kilivyoainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) kulipa ada ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kila mwaka ambao shughuli ya uchimbaji utakuwa ukifanyika kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii

(c) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hiii na masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi; na

(d) kulipa ushuru na tozo mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au sheria ndogo nyingine zilizotungwa na Halmashauri

Muda wa uchimbaji na masharti ya usafirishaji

6.-(1) Shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kila siku.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda ulioainishwa.

(3) Kila mmiliki wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa gari hilo limefunikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi.

Ushuru wa madini ya ujenzi

7.-(1) Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi ambao utalipwa na msafirishaji, mchimbaji na muuzaji wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumzuia msafirishaji, mchimbaji, muuzaji na kuzuia chombo cha usafirishaji kuuza au kusafirisha madini ya ujenzi kama ikibainika kuna ukiukwaji wa Sheria Ndogo hii.

Vituo vya ukaguzi

8.-(1) Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi katika njia zinazoingia au kutoka katika maeneo ya machimbo.

(2) Kila dereva wa chombo cha usafiri

kilichobeba madini ya ujenzi atatakiwa kusimama katika kituo cha ukaguzi na kuonesha stakabadhi ya kielektroniki ili kuthibitisha kulipwa kwa ushuru wa madini ya ujenzi yaliyo katika chombo cha usafiri.

(3) Chombo cha usafiri kitakachokamatwa kwenye eneo la machimbo na dereva au mmiliki wake akakimbia au kutoroka, chombo hicho hakitaruhusiwa kutoka mpaka kitakapolipiwa faini na ushuru unaodaiwa.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

9.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa halmashauri au wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

10.- Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote yanapochimbwa madini ya ujenzi kuanzia saa kumi na

mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa nia ya kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa uendeshaji wa shughuli za uchimbaji.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

11.-(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya ndogo ya (1), halmashauri kabla ya kufuta au kusimamisha kibali itatakiwa kutoa notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali kwa mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji.

(3) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu yeyote aliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atasimama kuchimba madini hayo.

Uteuzi wa wakala

12.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroni na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na halmashauri;

Makosa

13.- Taasisi, kampuni au mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii endapo-

(a) ataanzisha machimbo ya madini ya ujenzi bila kuwa na kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atasafirisha madiniya ujenzi bila kulipa ushuru;

(c) atachimba madini ya ujenzi kabla au baada ya muda ulioruhusiwa kuchimba;

(d) atasafirisha madini ya ujenzi katika gari ambalo halijafunikwa;

(e) atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa ushuru;

(f) atakataa kutii agizo lolote atakalopewa na afisa mwidhiniwa wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

(g) atakataa kulipa ushuru au kumzuia afisa

mwidhiniwa au wakala kutekeleza wajibu wake;

(h) atakwepa kulipa ushuru kwa kupita njia tofauti na kituo cha ukaguzi;

(i) atachimba madini katika maeneo yasiyoidhinishwa; au

(j) atachimba shimo kubwa kwa ajili ya madini na kuliacha bila kupanda miti au mimea mara baada ya madini hayo kumalizika.

Adhabu

14.- Mtu yeyote anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha makosa

Sura ya 290

15.- Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha makosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa mujibu wa Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa
T. S Na. 382 ya 2020

16.- Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020 inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(b))*

ADA YA UCHIMBAJI MADINI YA UJENZI

| NAMBA | AINA YA MADINI | KIASI CHA ADA YA KIBALI (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Madini yote ya ujenzi | 50,000/= kwa kila kibali |
| | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7 (2))*

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NAMBA | AINAYAMADINI | KIWANGO CHA USHURU (SHILINGI) | KIWANGO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchanga | 1500/= | $M^3$ |
| 2. | Kokoto | 1500/= | $M^3$ |
| 3. | Morum | 1500/= | $M^3$ |
| 4. | Udongo/Kifusi | 1000/= | $M^3$ |
| 5. | Mawe | 1500/= | $M^3$ |
| 6. | Matofali | 1000/- | $M^3$ |
| 5. | Magnesite | 1500/= | $M^3$ |
| 6. | Feldsper | 1500/= | $M^3$ |
| 7. | Bauxite | 2500/= | $M^3$ |
| 8. | Gypsum | 1000/= | $M^3$ |
| 11. | Shaba | 5,000/= | $M^3$ |

__________________

JEDWALI LA TATU

________________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi;…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya;……………………………………..…….ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, kwamba mnamo tarehe;……..... mwezi;…...................................…. Mwaka; ……..….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Aya ya …..….. ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU:

Leo tarehe;…....... ya Mwezi;………… Mwaka;…………..

Jina;………………………………..…………………….

Saini;………………………..……………………………

MBELE YANGU :

Jin;…………………………..……..……………………

Wadhifa;……………………………………………..…

Saini;…………………………………………………………

Tarehe;…………………………………………………….

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Same imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 05 mwezi Mei mwaka 2023, Mbele ya;

ANASTAZIA TUTUBA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

YUSTO M. MAPANDE(DIWANI)
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma
25 Machi, 2024.

MOHAMED OMARY MCHWENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*